*Namba ya Mtahiniwa …………………*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI**

**021** **KISWAHILI**

**Muda: 2:30** **Jumatatu, 11 Novemba 2019 asubuhi**

**Maelekezo**

maktaba.tetea.org

1. Karatasi hii in sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Majibu **yote** yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kaalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Vifaa **vyote** vya mawasiliano visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |


Find this and other free resources at [http://maktaba.tetea.org](http://maktaba.tetea.org)

## SEHEMU A (Alama 25)

## UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Katika miji mikubwa nchini Tanzania wimbi la ongezeko la watu bado ni kubwa. Ongezeko hilo la watu limesababisha kuzuka kwa matatizo makubwa maeneo ya mijini ikiwemo **msongamano** mkubwa wa magari na watu. Hali hii imesababisha wafanyakazi kuchelewa kazini, wanafunzi kuchelewa shuleni na hata wagonjwa kuchelewa kufikishwa katika vituo vya kutolea huduma za matibabu.

Hebu tujiulize, kwa nini watu wengi wanaondoka vijijini na kukimbilia mijini? Majibu yanaweza kuwa mengi, lakini miongoni mwa majibu hayo inaweza ikawa huduma zisizokidhi mahitaji ya kijamii. Jamii inatarajia kupata huduma bora za maji, umeme, barabara, matibabu, ajira na mawasiliano. Jamii inaposhindwa kupata huduma hizo katika **maskani** yao, lazima itafute huduma hizo nje. Na njia pekee ni kukimbilia mijini ambako huduma hizo zinapatikana.

Anasa pia ni sababu mojawapo. Ikumbukwe kuwa kundi kubwa la watu wanaokimbilia mijini na vijana. Kundi hili ni la watu wanaopenda starehe, hawataki kujituma na kujikwamua kimaisha, wanapenda kupata mafanikio ya haraka. Vijana wengi wanakimbilia mijini jambo ambalo linaleta wasiwasi wa hali ya maisha katika maeneo hayo ikilinganishwa na rasilimali zilizopo. Wengi wao hujiingiza katika vitendo vya uhalifu kama wizi na utumiaji wa madawa ya kulevya.

Ongezeko la watu mijini husababisha makaszi duni, uchafuzi wa mazingira na uhalifu wa kila aina. Ongezeko la watu katika maeneo ya miji linakwenda sambamba na ongezeko la magari hivyo tatizo la **miundombinu** isiyokidhi pia hujitokeza. Hali hii ikiachwa iendelee uharibifu wa mazingira utaongezeka kwa kiasi kikubwa kwa sababu watu watatafuta njia mbadala ili kuzitatua **changamoto** zinazowakabili.

**Maswali**

(a) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu hiki cha habari.

(i) Msongamano ……………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

(ii) Maskani …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

(iii) Miundombinu ……………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………



Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

(iv) Changamoto ..……………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(b) (i) Kulingana na kifungu cha habari ulichosoma ni kundi gani la watu hukimbilia mijini?
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(ii) Taja sababu mbili muhimu zinzowafanya watu wakimbilie mijini

- ……………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………..
- ……………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………..

(c) Ongezeko la watu mijini lisipodhibitiwa litasababisha nini?
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....

(d) Pendezeka kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu cha habari ulichosoma kisichozidi maneno matano.
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....

2. Andika ufupisho wa kifungu cha habari ulichosoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60).
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....


Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………………....

## SEHEMU B (Alama 20)

## SARUFI

3. Bainisha mzizi wa asili wa kila kitenzi katika sentensi zifuatazo:

(a) Mtoto anacheza mpira
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....

(b) Wanafunzi wanapigana darasani.
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....

(c) Sisi hatupendani.
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....

(d) Watoto walifungiana milango.
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....

(e) Vifaa feki viliharibiwa.
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....

(f) Mwalimu alitambulisha wanafunzi wageni.
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....

(g) Jana hatukusomeana.
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....



Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

(h) Mama alimuonesha baba daftari langu.
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....

(i) Mamia ya wachezaji wa Taifa Stars walipokelewa kwa shangwe.
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....

(j) Wakorofi walitolewa darasani.
……………………………………………………………………………………....
……………………………………………………………………………………....

4. (a) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

(i) Kidahizo
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(ii) Kitomeo
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(iii) Alfabeti
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(iv) Kamusi
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(v) Kitenzi
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(b) Bainisha aina ya nomino zifuatazo:

Mfano: Maji - nomino ya jumla/wingi

(i) Papai ..……………………………………………………………………………
(ii) Mungu……………………………………………………………………………
(iii) Arusha……………………………………………………………………………
(iv) Upepo……………………………………………………………………………
(v) Jumamosi ..………………………………………………………………………


Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (Alama 20)**

**MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA**

5. Onesha rejesta zifuatazo hutumika katika mazingira gani.

(a) Mimi kuku ugali moja, huyu wali maharage na wale pale Ng'ombe.
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(b) Zuia babu, kula hivyo vichwa vitatu.
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(c) Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kama ifuatavyo.
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(d) Ndugu Madongo Kuinuka unatuhumiwa kwa kosa la jinai la kuiba mali ya umma.
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(e) Jipatie mahitaji ya jikoni, nyanya, vitunguu, karoti, hoho, pilipili na ndimu vyote vipo.
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

6. Fafanua sifa tano za lugha ya kimazungumzo.

(a) ……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(b) ……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(c) ……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(d) ……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....

(e) ……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....
……………………………………………………………………………………….....


Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (Alama 30)

## FASIHI KWA UJUMLA

7. Eleza kwa ufupi dhima kuu tano za fasihi.

(i) ………………………………………………………………………………………....
………………………………………………………………………………………....

(ii) ………………………………………………………………………………………....
………………………………………………………………………………………....

(iii) ………………………………………………………………………………………....
………………………………………………………………………………………....

(iv) ………………………………………………………………………………………....
………………………………………………………………………………………....

(v) ………………………………………………………………………………………....
………………………………………………………………………………………....

8. Kamilisha methali zifuatazo:

(a) Hakuna masika ………………………………………………………………………
(b) Mchonga mwiko ……………………………………………………………………
(c) Chanda chema ..……………………………………………………………………
(d) Asiyefunzwa na mamaye ..…………………………………………………………
(e) Dalili ya mvua ..……………………………………………………………………

9. "Ngonjera ni maigizo na pia ni mashairi". Toa sababu tatu za kuthibitisha usemi huo.

(i) Ngonjera ni maigizo kwa sababu:

- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

(ii) Ngonjera ni mashairi kwa sababu:

- ……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………



Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

- …………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
- …………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

**SEHEMU E (Alama 15)**

**UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI**

10. Kwa kuzingatia hoja nne, andika insha isiyopungua maneno mia moja na hamisi (150) na isiyozidi maneno mia mbili (200) kuhusu Umuhimu wa Lugha ya Kiswahli.

…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....
…………………………………………………………………………………………....



Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org